AIMWA 009

# VINEYARD

## MUHULA WA III

## KISWAHILI DARASA LA SITA

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujaze nafasi zilizoachwa wazi kutoka 1-15.***

Kenya ni __1__ ambayo imebarikiwa kuwa na __2__ zaidi ya arubaini na __3__. Watu wa maeneo mbalimbali hufuata mila na desturi mbalimbali hasa __4__ kutoka kwa mababu __5__. Jamii inayohamahama huzingatia __6__ kwa sababu ni rahisi kuhama na mifugo. Wamaasai wanatambulika kila waendapo kwani hawakosi __7__ kiunoni na __8__ mkononi. Virungu hivyo wanavyovibeba ni silaha ambayo hawaitumii ovyo ovyo.

Jamii ya Wakaraba inasifika kwa ujuzi wa kurusha mishale. Si ajabu kuwaona wamebeba __9__ mikononi na mishale iliyojaa __10__. Ni rahisi __11__ adui kwa sababu unaweza kujificha mbali na mshale hautoi silaha. Serikali inashughulikia __12__ la __13__ wa mifugo. Jambo hili limesababisha __14__ mengi kwa sababu hakuna anayekubali kuwapoteza mifugo __15__.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | inchi | taifa | nchi | mahali |
| 2. | mataifa | makabila | kabila | majimbo |
| 3. | mawili | wawili | miwili | mbili |
| 4. | walioziirithi | walizoridhi | walizoziridhi | walizozirithi |
| 5. | zao | yao | wao | zako |
| 6. | ulimaji | ufugaji | ufungaji | ukulima |
| 7. | njora | mikuki | sime | mishale |
| 8. | gumbasi | ngao | mikuki | vimangare |
| 9. | uta | bunduki | nyuta | manati |
| 10. | ziakani | riaka | pongono | podo |
| 11. | kumfunga | kumpiga | kumtunga | kumfuma |
| 12. | swala | suala | sala | suhala |
| 13. | uibaji | wizi | uwizi | wezi |
| 14. | maafa | vifo | maiti | shida |
| 15. | wao | yake | yao | zao |

***Kutoka swali la 16 hadi 30 jibu kulingana na maagizo.***

16. Ni chakula gani ambacho hutokoswa?
   A. chapati
   B. chenza
   C. viazi vitamu
   D. bajia

17. ____________ ya vitabu yameloa chepe.
   A. Matope
   B. Makundi
   C. Matopa
   D. Kifurushi

18. Kamilisha methali hii:- Kikulacho ki ____________
   A. nguoni mwako  B. nawe
   C. nje  D. ndani yako

19. Andika kwa wingi:- Mkunga huyu ni mtamu.
   A. Kunga hizi ni tamu

B. Wakunga hawa ni watamu

C. Mikunga hawa ni watamu

D. Mikunga hizi ni tamu

20. Kamilisha sentensi ifuatayo kwa kuradidi:-

Mwanafunzi ____________

A. huyu huyu

B. yuyu huyu

C. hii hii

D. wawa hawa

21. Kikembe cha Sungura huitwaje?

A. Kisungura B. Kitungule

C. Kivinimbi D. Kiyoyo

22. Nitamwitaje mama wa mama yangu?

A. Shemeji

B. Shosho

C. Nyanya

D. Mama mkwe

23. Tumia kiunganishi sahihi kukamilisha sentensi hii:-

Baba yake Chuchi hakushiriki zoezi ________ kucheza mechi.

A. ila B. basi

C. lakini D. wala

24. Andika akisami hii kwa maneno $^{3}/_{9}$?

A. Tatu tusui

B. Thumni tatu

C. Tusui tatu

D. Ushuri tatu

25. Mwanajeshi alivalia __________ ili kuzuwia risasi kupenya mwilini.

A. Dereya

B. Kabuti

C. Gwanda

D. Mtutu

26. Kitendawili:- Ni mgeni wa kila mja japo hapendwi __________


A. kifo

B. mwiba

C. hela

D. shangazi

27. Hili ni umbo lipi?



A. Mistari sulubu

B. Mistari sambamba

C. Pembe tatu

D. Mishale

28. Chagua kiulizi sahihi kukamilisha sentensi:-

Ni mayai _______ hayaliki.

A. magani B. ngapi

C. yepi D. wapi

29. Anakoishi kuku ni kizimbani. Je, anakotagia kuku ni ____________

A. kizimba B. fuko

C. karai D. kata

30. Shairi lenye mishororo minne katika kila ubeti ni:-

A. tarbia

B. tarbushi

C. tarakilishi

D. tashtiti

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40.***

Shumbe alitumia hela nyingi kuwapa wazazi wa Nuru. Aliwasahau wazazi wake kabisa na mara nyingi alipopata barua kutoka kwao, alizirarua bila hata kuzisoma. Mambo yaliendelea vivyohivyo mpaka wakati wao wa kuoana ulipofika, ndipo wakafunga ndoa takatifu kanisani walipokutana mara ya kwanza.

Baada ya kuishi pamoja kwa mwaka mmoja hivi, Nuru alifanikiwa kupata mtoto wa kiume aliyemwita Paulo. Mtoto wao alilelewa katika hali nzuri ya maisha. Shumbe aliweka pesa nyingi sana za kumnunulia mavazi ya bei ghali. Hata gharama ya maisha yao ilikuwa ya juu sana ingawa wote wawili walikuwa walevi

kupindukia.

Shumbe alianza kuonyesha tabia mbaya sana katika kazi yake. Hakuifanya kazi yake vizuri tena. Ule uaminifu wake wa hapo awali ulianza kutoweka. Maisha yake yalizidi kuwa mabaya. Alianza tabia ya kuzunguka vibarua kila mahali mjini mara alipofika saa za jioni?Ilikuwa kawaida yake kutembelea jiji la Nairobi mara mbili au tatu kwa siku.

Alichelewa kufika kazini, hakuwa na mtu mwingine ambaye angeshika kazi yake wakati yeye mwenyewe hayupo. Kwa hivyo vitu vingi vya Kampuni hiyo viliibwa na wafanyikazi. Alizidi kuzururazurura mjini na mara nyingi alichelewa kufika nyumbani kwake mpaka saa nane au tisa za usiku. Mwishowe alipigwa kalamu kazini naye bibi akapotelea kwao kwani hawangeweza kumvumilia tena. Maskini Shumbe, ole wake!

---

31. Waliopokea hela nyingi kutoka kwa Shumbe ni:-
   A. Nuru
   B. Wazazi wa Shumbe
   C. Shumbe
   D. Wazazi wa Nuru

32. Waraka aliopata Shumbe kwa wazazi wake ali ___________
   A. soma
   B. rarua baada ya kusoma
   C. chomoa
   D. rarua bila kusoma

33. Ni nani aliyekuwa mlevi?
   A. Nuru
   B. Hakuna
   C. Shumbe
   D. Nuru

34. Kupigwa kalamu ni ___________
   A. kufutwa kazi
   B. kupata kazi
   C. kupigana na kalamu
   D. kuajiriwa kazi

35. Shumbe pamoja na Nuru walikuwa na watoto wangapi?
   A. Wanne
   B. Mmoja
   C. Sufuri
   D. Watatu

36. Nuru alipotelea kwao maana yake ni ___________
   A. alikimbia mbio
   B. alitoka kwenye ndoa
   C. hajulikani alikopotelea
   D. alipotea kwa njia

37. Mtoto alinunuliwa vitu vya bei, ni sawa na kusema:-
   A. vitu vya thamani
   B. vizee
   C. rahisi
   D. vikuukuu

38. Ni nini kilichosababisha Shumbe kuacha kazi?
   A. Mke
   B. Wazazi
   C. Pombe
   D. Wezi

39. Kila mara Shumbe alifika nyumbani saa gapi?
   A. Usiku wa manane
   B. Kuelekea kukucha
   C. Asubuhi
   D. Jioni

40. Kwa maoni yako, adhabu aliyopewa Bwana Shumbe ilimfaa?
   A. Ndiyo
   B. La
   C. Hapana
   D. Si sana

***Soma habari hii kisha ujibu maswali yafuatayo.***

Vile tunavyozidi kukua ndivyo tunavyoendelea kujifunza mambo mengi maishani. Kati ya hayo, muhimu zaidi bila shaka ni kazi na mapumziko mbali na pilkapilka nyinginezo.

Kuna kazi za aina nyingi. Hata hivyo, wajibu wetu mkubwa ni kuwasaidia wazazi kwa kazi kama vile kufua nguo, kuchunga mifugo, kutumwa dukani na kufagia.

Lakini inasikitisha kuwa wengi wetu hupendelea uvivu na kucheza. Uzembe una ndugu yake katika kujisingizia ugonjwa, nako kucheza hakuwezi kutulisha wala kutuvisha.

Ndivyo tunaambiwa kuwa uvivu ni adui wa maendeleo, kwamba zile kazi, vikazi na vijakazi nyumbani ndivyo michango yetu katika kutafuta riziki.

Kupumzika kama sehemu nyingine ya maisha yetu hakuna haja kuzungumziwa sana. Kwa nini tupumzike? Hata katika maandiko matakatifu tunaendelezwa kuwa katika kuumba ulimwengu, Mwenyezi Mungu alifanya kazi kwa siku saba. Sisi pia hadi kadhalika tuna siku ya kupumzika kila juma.

Katika kufanya kazi huwa tunatumia nguvu. Kitumiwacho humalizika. Lakini kwa bahati nzuri nguvu zetu hujengeka na kupatikana upya baada ya mapumziko. Matokeo yakiweza kufanya kazi vizuri na kwa moyo zaidi.

41. Vijana huendelea kukua ___________
    - A. urefu na unene
    - B. urefu na kiakili
    - C. kenenepa tu
    - D. kimwili na kiakili

42. Neno pilkapilka linamaanisha?
    - A. Shughuli chache
    - B. Kazi
    - C. Heko
    - D. Shughuli mbalimbali

43. Njia nyingine ya kusaidia wazazi wetu ni:-
    - A. kulala
    - B. kulalama
    - C. kutumwa
    - D. kuchunga wanyama mwitu

44. Kisawe cha neno uzembe ni ___________
    - A. upotevu
    - B. utepetevu
    - C. kula
    - D. uvivu

45. Kutokana na habari Mungu pia ___________
    - A. alipumzika
    - B. huzembea
    - C. hulala
    - D. hachoki

46. Neno riziki kulingana na habari hii ni:-
    - A. chakula
    - B. usingizi
    - C. gange
    - D. bahati

47. Ni jambo gani halijapendekezwa?
    - A. Kulegea
    - B. Kupumzika
    - C. Kufanya kazi
    - D. Kula

48. Kamilisha kulingana na hadithi:- Uvivu ni ______
    - A. duwaa
    - B. ugonjwa
    - C. uzembe
    - D. adui

49. Sababu maalum ya kupumzika ni ___________
    - A. kuendeleza uzembe
    - B. kukua kimwili
    - C. kuona raha
    - D. kupata nguvu mpya

50. Mungu alifanya kazi siku ngapi?
    - A. Tisa
    - B. Saba
    - C. Sita
    - D. Moja